Hali ya anga ilikuwa tulivu kabisa, ni utulivu uliofanana na asubuhi ama jioni lakini sikumbuki vizuri yaani sifahamu ni wakati gani huo, kwa mbali tu nilisikia mingurumo ya vyombo vya moto kwa sababu barabara nayo ilikuwa mbali.

Kwa ufupi nyumba ninayoishi ilijitenga kidogo na mji lakini karibu na nyumba zingine. Kwa hiyo si kwamba nyumba niliyoishi ndio ilijitenga lakini ni mtaa ndio ulijitenga na mji. Sauti pekee nilizosikia ni za watoto wa nyumba za jirani wakicheza michezo yao ya kitoto na mara chache nikisikia sauti za watu wazima wakizungumza au kuwaita watoto wao majumbani. Mradi pilikapilika na kila mmoja na lake.

Ndio hali halisi niliyokuwa napitia, wakati wapo waliokuwa wakifurahia maisha kwa upande wangu ndani ya nyumba yangu kuukuu nilikuwa katika ulimwengu wa peke yangu kabisa. Ulimwengu mgeni nisiouzoea na hali ya kutouzoea ndio inayonipelekesha puta sasa, maisha yangu yalitengeneza sinema ambayo kama angalikuwapo mwongozaji mahiri yeyote na popote duniani akaiweka katika mfumo wa sanaa za maonyesho angejizolea sifa kedekede.

Nilitoka chini, nikapanda mpaka juu kabla sijashuhudia anguko la ghafla ndani ya kitendawili kizito, anguko la ajabu nisilofahamu msingi wake haswa mpaka wakati huu. Ni maanguko ya namna hii ambayo wengi wenye kushindwa kuhimili hisia za ndani huishia kujidhulumu nafsi ilimradi tu akili na nafsi zao zisishuhudie fedheha, dhihaka na kila aina ya aibu inayoambatana na maanguko yao.

Wakati tafakuri hizi zikipita kichwani mwangu nilikuwa ndio natoka kuyafungua macho baada ya kupoteza fahamu kwa masaa mengi nisiyokumbuka, si kwa kuzirai ama vinginevyo bali kwa kilevi kingi nilichobugia siku iliyopita kabla sijakata fahamu. Hata hivyo sina hakika kama ni siku iliyopita ama vinginevyo, sina kumbukumbu nzuri kutokana na masaibu yangu na aina ya maisha ninayoishi kwa sasa.

Pamoja na uchovu mwingi lakini njaa nayo haikuacha kuniandama, sikuwa na nguvu mwilini hivyo nikajikokota kuinuka angalau nilipatie chochote tumbo langu. Nikajiinua kwa tabu na kukaa kitako katika kingo za kitanda changu kidogo chenye ukubwa wa mita nne kwa pande zote, cha mbao. Nikamudu kuinuka na kuketi lakini bado nikafeli kusimama kwa mfululizo, maana kichwa kilipitiwa na kizunguzungu kidogo cha ghafla nikainamisha kichwa kiasi kisha kiganja changu cha mkono wa kulia kikavinjari maeneo yote ya kichwa. Nikafikicha macho kwa uchovu mwingi nisioelewa ni wa mawazo, njaa ama ulevi. Ulikuwa mchanganyiko wa kusikitisha tu ukinisulubu bila huruma katika ulimwengu huu dhalimu.

Mkono wangu wa kushoto ulikamata ukingo mmoja wa kitanda ili kupata uwiano sawa. Mkono wa kulia uliokuwa ukipapasa kichwani ndio ulibaini nywele zangu za kipilipili zilizojiotea bila busara, haraka fahamu zangu zikayaelekeza macho kujaribu kuvinjari maeneo yote ya mwili ambayo yangefika. Ni kwa mara ya kwanza nikabaini namna afya yangu ilivyozorota, nimedhoofu, vijana wa mjini wanasema 'nimepoteza'. Nimeshapoteza ramani ya vita sasa natangatanga bila uelekeo.

Nikazikusanya nguvu na baada ya kujihakikishia sasa naweza kusimama basi nikanyanyuka, ukafuata mwayo mrefu kabla sijajinyoosha kuweka sawa mwili. Na kabla sijafanya lolote nikakumbuka sijashika simu yangu kwa muda mrefu, nikageuka nyuma na kutazama katika kona moja ya kitanda ambako nilitegemea ningeiona, kwa kawaida nina desturi kila ninapolala basi simu ningeiweka karibu na mto wa kulalia, yaani kichwani. hiyo nilikuwa napoteza kila kitu. Haikuwepo. Kichwa kikapata moto maana kwa kuipoteza simu

Nikarudisha shingo yangu mahali pake kama awali kisha nikafikicha uso wangu ambao hata hivyo bado haukupitishwa maji. Mbele yangu ukutani palikuwa na kioo kidogo nikakitazama kwa muda, taswira yangu iliyoonekana kupitia kwenye kioo ilinirudisha mbali sana kihisia, kabla sijakuwa Almasi huyu wa sasa. Nikapiga hatua chache kukisogelea kisha nikasimama mbele yake. Nilikuwa kifua wazi lakini chini nilivaa suruali ngumu aina ya *jeans* kwa maana kwamba nililala na suruali!

Mbele ya kioo nilikuwa natazamana na mimi mwenyewe. Nikatumia muda huo kujitathimini kupitia kioo hicho kuanzia utosini mpaka maeneo ya kifua ambako ndio mwisho wa urefu wa kioo hicho. Ama hakika kweli nilipoteza mwelekeo. Nilikaa mbele ya kioo kwa takribani dakika kumi bila kusemezana chochote na mimi wa kwenye kioo. Sifahamu ni kwa nini lakini nilijikuta nikiangusha tabasamu, ambalo kimsingi si la furaha wala matumaini bali lenye tafsiri ya ushindi ambao haijulikani lini utadhihirika. Ushindi kuhusu nini? Nashindana na nani? Sijui.

"Hii ni vita ya nafsi, vita mbaya sana isiyotajwa" nikajisemesha nikishusha pumzi ndefu bado nikiendelea kusalia mbele ya kioo nikipitisha kumbukumbu mbalimbali zilizokuwa zinakuja na kukata harakaharaka utadhani zinafanya hadaa na nafsi yangu pweke.

Kwa ufupi huyu niliyekuwa namtazama sasa sio mimi yule wa miezi kadhaa nyuma, na nilipokuwa nikiendelea kusimama mbele ya kioo nikasikia mlio wa simu yangu kutokea katika kona nyingine ya kitanda. Ilikuwa kwenye muito wa mtetemo.

"Mungu mkubwa!" nikajisemea kwa sauti ya chini maana niliamini simu nilishaipoteza ulevini kwa kuwa sikumbuki nilifika vipi nyumbani wala saa ngapi. Kumbe nilipotupia shati baada ya kuvua ndipo simu ilipokuwa, haraka nikapiga hatua kuifuata nikafunua shati, simu ilikuwa chini ikiendelea kuita.

Nikatazama mpigaji, alikuwa mama yangu, nguvu zikaniisha. Kwa makusudi

matupu sikutaka kuipokea maana ni wiki sasa mfululizo anapiga sipokei sio kwa kupenda lakini ni kwa sababu angetaka kusikia kutoka kwangu shida ni nini na mimi siko tayari kumwambia. Fedheha inayonikabili sikuweza kuibeba.

Nilikuwa nikipambana kumalizana na kadhia inayonikabili ili wakati mwingine akipiga niwe tayari kuipokea nikiwa na majibu. Katikati ya hii fedheha inayoendelea sikuwa na chochote cha kumwambia na pengine akijua yale yaliyonipata huenda ingeharakisha kifo chake kutokana na mgogoro wa afya anaopitia pia. Sikutaka hili litokee wala sikutaka niwe chanzo cha kifo cha mama.

Nikaendelea kuitazama simu kwa kitambo ikiita tu mpaka ikakata, kabla sijairudisha mahala pake ikaanza kuita tena. Sikuipokea vilevile!!

Ilipokata nikabofya namba kadhaa kuipigia simu nyingine ikaita kidogo ikakatwa.....!!!

“Nimekwisha” nikajisemea.

Nikatoka ndani ya chumba changu taratibu na kujielekeza katika chumba kingine cha uani, hicho anaishi mwanadada mmoja mlalahoi mwenzangu ambaye riziki yake inategemea kudra za miguu yake kupitia biashara ndogondogo za kutembeza mitaani. Sabrina, huyu ndio alikuwa mkombozi wangu kila ninapokwama. Mara nyingi alipopika chakula basi huja kunigongea mlango ili tugawane umasikini. Na siku zote nilikataa kukwepa kumuongezea mzigo usio na tija lakini leo njaa ilinikamata penyewe, minyoo ya tumbo ilisakata rhumba vilivyo kwa hivyo sikuwa na namna zaidi ya kujisalimisha kwake!

Pupa zikaniisha nilipokutana na kufuli zito mlangoni kwake, hayupo. Alishajihimu mapema kabisa kuwahi mihangaikoni. Nikahisi vile nitakavyokiona cha mtema kuni siku ya leo, taratibu nikaketi kitako katika ngazi za mlango wake. Kama ni mwambo huu umetakata!

Naitwa Almasi Hobela.

****

M

ahali fulani jijini Dar Es Salaam, jiji lililosheheni raha na karaha, jiji ambalo watanzania wengi wanaotokea mikoa mingine ndoto zao ni kulikanyaga kwa namna iwayo yote, iwe kwa matembezi ama kwa shughuli mbalimbali. Naam jiji lililochangamka vya kutosha. Sura ya Tanzania.

Ni katika baa iliyofahamika kama Micasa Lounge maeneo ya Ubungo, napo mambo yalikuwa moto, Jumamosi hii palifurika mapema sana. Wateja mbalimbali walijazana mahali hapa wakizipatia roho zao kile zinataka kwa nafasi zao kulingana na matakwa. Wenye kushibisha matumbo yao walifanya hivyo na wale wenye kuhusudu vinywaji basi wangepata iwe vile baridi au vilevi ili mradi kila mmoja kwa wakati wake alijitahidi kufanya kile kilichomfikisha mahali hapo.

Bendi moja isiyo maarufu iliendelea kutumbuiza taratibu kwa kuiga nyimbo na mitindo maarufu na isiyo maarufu. Bendi hii japokuwa haikufahamika lakini ilijengwa na wanamuziki mahiri kweli waliofanikiwa kuzikonga nyoyo za wateja vilivyo. Mteja yeyote aliyeguswa na wimbo wowote angekwenda kuwatuza bila pingamizi ama aliyehitaji wimbo aupendao upigwe angeomba kwa dau dogo tu. Raha rahani.

Bado ilikuwa mapema tu yapata saa mbili hivi juu ya alama jioni. Katika meza moja ya zile zilizokuwa katikati kati ya meza zingine walikaa watu wawili wa jinsia mbili tofauti. Mwanaume na mwanamke wote vijana kabisa wakiendelea na mazungumzo yao yaliyoonekana kuwa na unyeti wa aina yake kutokana na namna walivyoilinda meza yao kila mtu baki alipokaribia kuvamia himaya yao. Hawakutaka kuungana na mtu mwingine hapo mezani pamoja na kwamba vilisalia viti viwili vitupu katika meza yenye viti vinne.

Watu hawa wawili pekee ndio hawakuwa wakitumia chochote si chakula wala kinywaji, hata mhudumu alipozuru meza yao hawakuonyesha nia kuhitaji huduma. Hali ikaendelea hivyo kwa muda mfupi kabla hajaongezeka mwanadada mwingine mwenye wajihi wa 'kimjini mjini' kuungana watu hawa mezani pao, ni dhahiri kwamba ndiye waliyekuwa wakimsubiri kwa muda wote huo ndio sababu hawakutaka aongezeke mtu mwingine kwenye viti viwili vilivyobaki vitupu asiye katika mpango wao. Mwanadada huyo alipofika eneo hili akatumia muda mfupi akiangaza huku na kule alipowatambua wenyeji wake akajongea katika meza yao na kuketi, yeye pia hakuagiza chochote kama ilivyokuwa kwa watangulizi wake na alionekana mwenye haraka sana. Aliketi mbele ya meza akitazamana na wenyeji wake huku ameipa mgongo bendi ambayo iliendelea kutumbuiza taratibu kwa

kuchanganya mahadhi.

Baada ya kutulia katika kiti chake mazungumzo yao yakashika hatamu. Kwanza alianza kuzungumza dada huyu mjanjamjanja, aliongea kwa haraka alipomaliza akaacha nafasi kwa wenyeji wake kuzungumza yao. Ni mazungumzo ambayo hakuna aliyeyasikia kutokana na pilikapilika za mahali hapa zenye kumfanya kila aliyepo kujali zaidi mambo yake, isitoshe watu hawa watatu walihakikisha hakuna mtu mwingine zaidi yao angesikia mazungumzo yao, kuna wakati iliwalazimu kuinama kidogo na kusogeleana ili kusikilizana vyema au wakati ambao mhudumu angefika jirani nao wangesitisha mazungumzo mpaka pale akishaondoka wanaendelea tena.

Mazungumzo yakaendelea katika umakini uleule na sasa yule dada alionekana kama anayepokea maelekezo fulani kutoka kwa wenyeji wake. Dakika kumi tu tangu yule mwanadada afike mahali hapo zilimtosha kufanya kilichomleta hivyo akainuka na kuondoka. Wenyeji wake walipohakikisha ameshatokomea hawakudumu kwa muda mrefu wakaondoka pia!

****

Majira ya saa kumi na moja alfajiri ghafla usingizi ulikata, macho yakafunguka kutoka katika usingizi wa pono katika namna ya mazoea ya mwili tu kwa vile ndivyo nilivyouzoesha. Kwa wakati huu sikuhitaji kengele ya simu yangu kuniamsha, pengine ingeniamsha wakati ule, siku za nyuma kabla haijakuwa desturi yangu. Lakini kwa muda mrefu sana baada ya kuamshwa nayo nilijikuta mwili ukifanya mazoea na ningeweza kuamka bila mlio wake. Sasa ni kawaida kabisa kengele kuita nikiwa tayari nimeshaamka kitambo hata hivyo sikutaka kuifunga kengele ya simu yangu ati kwa kuwa haina msaada tena, la hasha niliiacha iendelee na utaratibu wake wa siku zote kwa tahadhari ikiwa ubongo wangu siku hiyo utachoka sana na kusahau jukumu lake basi kengele ingetekeleza wajibu wake.

Katika hali ya kawaida nikishaamka kwanza hupekua simu yangu kuona kama kuna ujumbe wowote uliingia usiku kisha hukamata kitenda mbali almaarufu *'remote control'* ya runinga ili kufuatilia taarifa mbalimbali za ulimwengu mapema kabisa. Ndivyo ilivyokuwa asubuhi hii.

Nikaendelea kusikiliza taarifa katika runinga huku nikiendelea kuperuzi simu yangu katika namna ya kuokoa muda maana kama ingebidi kila kimoja nikifanye kwa wakati wake basi ningepishana na ratiba yangu. Katika simu nilipitia mitandao yote kabla sijamalizia na mtandao mmoja pendwa sana ambako huko nilikutana na ujumbe katika kasha, nikaufungua. Halikuwa jambo geni kwangu kukutana na jumbe mbalimbali tena nyingi sana kutokana na shughuli zangu na mafanikio yangu yaliyonigeuza fursa adhimu kwa vijana wanaoendelea kupambania hatima zao.

Kati ya jumbe hizo kuna ambazo hazikuwa na mantiki kabisa lakini sikuwa

mpuuziaji, mara zote ningejitahidi kuzipitia kwa haraka na kuweka umakini katika zile muhimu tu.

Leo haikuwa kawaida, hapakuwa na jumbe nyingi sana pengine ndio sababu nilipata muda wa kupitia ujumbe huu. Ulikuwa ujumbe wenye maelezo marefu kiasi yenye kumalizia na mawasiliano ya namba za simu pekee. Kwanza nilipuuza, lakini baada ya kufikiri kidogo nikasitisha puuzo.

"Matapeli?" Nilijiuliza nikiinuka kitandani.

"Hapana sio matapeli" akili yangu ikanipinga nikivuta hatua ndogo zisizo na malengo ndani ya chumba hicho, niliinuka tu kitandani pasipo na maamuzi iwapo naelekea maliwatoni ili kujiswafi ama nanyoosha nguo zangu kwanza. Yaani kipiki aanze kabla ya kipi?

“Watu makini hawawezi kuzungumza *‘deal’* kubwa hivi kupitia mitandao, nilitegemea kama walinikosa kabisa basi huko mtandaoni wangeomba anuani ama mawasiliano na mambo mengine yakazungumziwa ofisini” nikajiuliza.

“Si ndio sababu wameacha namba zao za simu!” akili yangu ikanijibu. Na kwa ushawishi wake ilielekea kunishinda, Nikaliweka kiporo.

Nikajinyoosha na kuachia mwayo wa kizembe. Nikasimama katikati ya chumba, nikipata mtanziko usioeleweka wa nini nataka nifanye kwa wakati huo. Sikuwa na mashaka yoyote dhidi ya ujumbe ule, hakika hapakuwa na shaka kabisa, haukuwa ujumbe wa kutisha wala wenye viashiria vya hatari yoyote kwangu. Ni masuala ya kibiashara tu ila namna ya uwasilishaji wake ndio iliyonishtua kama sio kunishangaza.

"Hata hivyo si lazima sana, unaweza kuachana naye tu, hilo liko ndani ya uwezo wako?" akili yangu iliendelea kufanya mdahalo usio rasmi na mimi.

"Hapana!" nikaijibu kwa ufupi nikielekea maliwatoni. Nilifanya yafanywayo humo nikatoka nikiwa safi kabisa tayari kwa kuvaa na kuondoka zangu.

Mimi bado ningali kijana wa miaka takribani thelathini tu, ni mjasiriamali ninayeelekea kukua, kwa hatua niliyofikia sijihesabu kama mwenye mafanikio lakini kwa upande wa vijana wanaoshinda vijiweni wakibishania mafanikio ya watu maarufu hasa wanamuziki au wanasoka basi wangeniona nina mafanikio makubwa, wao wanaita 'kutoboa' kwa upande wangu haikutosha kuvimba kichwa namna hiyo. Niliona safari yangu bado ndefu.

Namiliki ofisi ndogo ya wastani tu katikati ya jiji na mtu pekee niliyeajiri hapo ofisini ni dada mmoja tu ambaye ni katibu mukhtasi ili kuratibu shughuli ndogondogo za ofisi, yeye anaitwa Juliana mimi humwita Jully. Dada wa 'mjinimjini' sana, kama ungemtazama haraka ungedhani hafai kwa mahusiano ya kawaida wala

hafai kwa ndoa kitu pekee nilichompendea ni vile anaelewa wajibu wake awapo kazini.

Ajabu ni kwamba kutokana na hulka yangu tangu nifungue ofisi hii muda mfupi uliopita usiozidi mwaka mmoja na miezi kadhaa tayari nimeshawaachisha kazi 'madada' zaidi ya wawili niliowaajiri hapo kwa shughuli hizo lakini sio kwa upande wa Jully, yeye tulielewana. Wale wasaidizi wa awali ambao kwa haiba ya nje walionekana kuwa na nidhamu na maadili haikuchukua miezi sita kabla hatujavurugana na kila mmoja kuchukua uelekeo wake, siku zote watakuja kama watu sahihi wakishazoea ofisi wanataka waingie uvunguni kwa bosi, mimi.

Hasa kwa kuwa walijua sijaoa.

Wao waliamini mapenzi ni silaha kubwa kuendelea kubaki ofisini badala ya kazi, Hawa sikuona kama wako safari moja na mimi isipokuwa ni wababaishaji tu.

Sio kwa Jully, kwake suala tu la kuvaa nadhifu kuendana na ofisi ilikuwa shughuli pevu, mwanzo niliamini ndiye msichana pekee atakayedumu kwa muda mfupi zaidi ofisini hapo. Haikuwa hivyo, nilikosea.

Alipokea maelekezo kwa haraka na alipojua nataka nini hakukosea tena mahali pengine popote kuhusu kazi na wajibu wake, ikawa kazi na yeye, yeye na kazi. Muda wa kutegana tegana haukuwepo. Hizo habari hakuwa nazo kabisa, wenzake waliomtangulia waliongea kwa unyenyekevu na mimi kama bosi lakini yeye aliongea na mimi kama rafiki, nilitokea kumpenda kwa sababu aliishi vile nilivyotaka.

Baadaye nikaja kugundua ilikuwa janjajanja yake, hakutaka kuniogopa alitaka kuwa huru, hakutaka kunihofia alitaka kunizoea. Hatimaye tulikuwa marafiki. Tukashibana.

Wazo kuhusu ule ujumbe niliokutana nao asubuhi hii katika simu lilipotea pasipokujulikana, sifahamu kama nilimpuuza, lakini nafikiri sikumpuuza kama ndivyo basi alijipuuzisha mwenyewe. Kosa lake ni ujumbe wake uliponitaka nikipata muda nimtafute kwa namba yake ya simu aliyoambatanisha mwisho wa ujumbe wake. Maana yake ni kwamba hata baada ya siku, wiki, mwezi ama mwaka nikipata muda nimtafute itategemea na busara yangu.

Halafu iweje yeye aje na mpango mkakati halafu mimi ndio niwatafute? Tena nikijisikia, Sikuona kama mtu huyu alikuwa makini na mpango wake.

Baada ya kujiandaa kwa mtoko wa kimajukumu nikajitosa ndani ya gari yangu aina ya Carina kuelekea ofisini kwangu. Kawaida yangu baada ya kutoka nyumbani ndipo sasa huanza kupiga simu nikiwa garini kwa maana kwamba kwa muda ambao naamka sio rahisi kumpigia mtu kutokana na pilikapilika za maandalizi kuwahi majukumu na ninakuwa tayari ofisini kutokana na shughuli za hapana pale ugumu wa kuzungumza na simu hasa zenye nia ya salamu na mazungumzo binafsi

unarejea tena, ndio maana mara nyingi huwa natumia ule muda napokuwa njiani kuelekea kazini kwangu kuongea na simu.

Sasa siku zote mtu wa kwanza huwa mama yangu mzazi niliyemuacha huko Pawaga, jimbo la Isimani, mkoani Iringa. Mama yetu ametuzaa watatu tu, mimi nikiwa moto wa kwanza na wadogo zangu wawili wa kike. Mdogo wetu wa mwisho ni mdogo sana ana umri wa miaka kumi sasa. Mimi ndio tegemeo kuu kwenye familia yetu, baada ya baba yetu kufariki nikiwa na umri wa miaka kumi na nne ni mama yetu aliyebeba jukumu kutusomesha mpaka nilipofika kidato cha sita.

Nilijitahidi kusoma kwa bidii maana mama alikuwa akinisisitiza kwamba urithi pekee anaoweza kutupatia ni elimu na ni elimu pekee itatukomboa sisi na familia yetu. Alisisitiza zaidi hasa mimi ambaye ndiye wa kwanza kuzaliwa na ndiye mtoto wa kiume pekee, alisema mimi ndio baba yao, mimi ndio kichwa cha familia na natakiwa kuonyesha njia ya wadogo zangu.

Alinijenga kuamini mimi ndiye nitakayeikomboa familia yetu kutoka katika lindi la umasikini, kufaulu kwangu ndio ahueni kwa familia na kinyume chake.

Sikumuangusha, niliishi nasaha zake, niliziishi ndoto zake na nikayaishi matamanio na maono yake naye hakuacha kunipa moyo kila nilipofanya vizuri na hata pale ilipotokea nikayumba alinipa moyo. Nilisoma kwa bidii nikiamini katika elimu mpaka nilipofika kidato cha sita. Matokeo yalipotoka nilifanya vizuri sana, hali iliyopelekea nipate nafasi ya kuendelea na elimu ya juu kwa maana ya chuo kikuu.

Ni hapo ghafla mawazo yalipobadilika kwa nia njema, pepo la maisha likanikumba, pepo la pesa. Si kwa ubaya. Wala halikuwa wazo lililokuja ghafla, lilikuwepo tangu muda mrefu hasa baada ya mama yangu kuanza kusumbuliwa na maradhi ya moyo wakati huo nikiwa kidato cha tano, nilifikiria mambo mengi hasa kwa namna niliyoaminishwa kwamba mimi ndio jicho la familia na kwamba nimebeba hatima ya baadaye ya wadogo zangu. Nikafikiria itakuwaje mama yangu akianguka ningali bado sijapata msingi imara wa kimaisha, na kwa wakati huu ambao ameanza kusumbuliwa na maradhi nafikiri ndio ulikuwa wakati sahihi anaohitaji msaada wangu.

Kuacha shule kidato cha tano haikuwa na mantiki, nikaonelea ni vyema nijikongoje mpaka nimalize kidato cha sita halafu baada ya hapo nitasimamisha masomo kwa kuwa elimu ya chuo kikuu inatoa fursa kuendelea nayo wakati wowote anapokuwa tayari, huu ndio ukawa mpango ambao ulibaki kuwa siri, siri yangu peke yangu.

Wiki moja kabla ya kuripoti chuo (Chuo kikuu cha Dar Es Salaam, wakati huo vyuo vikuu vilikuwa vichache na waliochaguliwa walikuwa wachache vilevile kwa hiyo mara nyingi wengi walichaguliwa kusoma hapo) nilimfuata mama yangu. Ilikuwa jioni moja ya siku nisiyoikumbuka tuliketi kama familia tukiota moto na kupiga soga

"Mama siendelei na shule" nilisema baada ya utangulizi mrefu uliosheheni konakona nyingi kupata uhalali wa mawazo yangu.

Jinsi mdogo wangu wa mwisho alivyoshtuka kwa maneno yangu haya nikaelewa kipimo cha mshtuko wa mama, kama mtoto wa miaka kumi ameshtuka namna hiyo itakuwaje kwa mtu mzima kama mama yangu tena aliyejitoa kwa kila hali juu yangu akitegemea siku moja nitasimama nimsimamishe? Nikaanza kujutia kwa uamuzi wangu wa kuyaropoka haya, mapigo ya moyo yakataka kubadili utaratibu wake nikafanikiwa kuyadhibiti. Nikavuta pumzi na kuzishusha, nikamtazama mama kwa kituo namna alivyoingia hamkani. Aliuliza neno moja tu;

"Almasi unasema!?" Sikujibu.

Nikamtazama tena, macho yetu yalipokutana nikababaika kidogo na kuyakwepesha nikamtazama mdogo wangu anayenifuata naye pia macho yake yaliongea lugha moja na ya mama, nikahamishia macho kwa mdogo wangu wa mwisho kabisa yeye ndio alinichanganya kabisa, kwa umri wake kugundua upumbavu ninaoongea ni jambo la kutisha. Akili yangu ikataka kuvurugika huku nikipambana nayo ichukue utulivu wake kabla sijaharibu mambo na dhamira yangu kuyeyuka, jambo ambalo sikuwa tayari.

Mama amekuwa akinisisitiza kwamba mimi ni mwanaume, mwenye kujiamini na asiyesita katika maamuzi yake na kuyasimamia. Kama haitoshi uanaume unakwenda sambamba na ujasiri. Ndio nasaha ziliniivisha nikaiva almanusura kuungulia.

Hicho anachonishangaa nacho sasa ameshasahau ni zao la nasaha zake, niliamua kuvaa uanaume alionibatiza tangu ningali kinda.

Sasa niliweka maoni yangu mezani na ujasiri juu kusimamia maamuzi yangu kwa namna yoyote ile ambayo wazo langu litakumbana vikwazo.

*"Kabla hujaamua jambo jiridhishe iwapo umeamua kwa dhati ili kuepuka majuto, maana mtoto wa moto majivu. Kama umeridhika na maamuzi yako usiogope"*

Sauti iliyonipa jeuri ikasikika ndani yangu, na hakika nilirejewa na nguvu angalau maana kusema ule ukweli hali ilikuwa tete.

Wakati huo bado wote watatu wananitazama mimi tu, nafahamu hawa wadogo hawawezi kusema chochote walisubiri mama atie neno maana ndiye mtu mzima pekee aliyenizidi umri hapa. Sasa sijui kwa upande wake mama kimya chake alikuwa anafikiria nini juu yangu.

Kimya kikaendelea kutanda kwa dakika kadhaa kabla machozi hayajaanza kufunika mboni za macho yake taratibu.

"Mwanangu umerogwa?" Ndio alichoweza kusema.

Na alistahili kusema hivyo, wakati ule elimu ilikuwa ndio habari, mtoto kusoma chuo kikuu ilikuwa fahari isiyo mithilika. Ni wakati ambao mtu angeweza kurogwa tu kwa sababu ana mtoto anayesoma chuo kikuu. Ndio sababu mama yangu alipambana na kadhia kadha wa kadha za maisha ndoto zake kubwa zikiwa ni siku moja aje kuheshimishwa na sisi wanae, zile dhihaka za umasikini kutoka kwa watu kijijini hapo aliamini kuna siku zingewarudi mwanae atakapofika chuo kikuu na hatimaye kuajiriwa.

Mbaya zaidi mama alishaonja utamu wa heshima ya kuwa na mtoto msomi pale nilipohitimu darasa la saba na kujikuta nimefaulu na kuwa mmoja kati ya wanafunzi wachache waliopata nafasi kuendelea na elimu ya juu, halafu nikamvimbisha kichwa kidato cha nne, nikafanya vizuri tena kidato cha sita. Fahari iliyoje, wale aliowaita wabaya wake walishakata ngebe kitambo.

Halafu leo ikiwa ameshamtafuna ng’ombe mzima anasikia mwanae tegemezi sitaki tena shule, akili yake moja kwa moja ikampeleka kwenye ulozi. Ndio, ni uchawi tu na alikuwa sahihi kabisa kwa kuwa halikuwa jambo la kawaida kiasi kwamba hata mimi mwenyewe nilipokuwa nikijitathimini kuna wakati nilidhani huenda kweli nimerogwa! Mama aliamini ‘watu wabaya’ wameamua kunichanganya mwanae ili kuvuruga mtiririko wa maisha yangu.

Baada ya hapo zilifuata nasaha ndefu sana akikumbusha shida zote tulizopitia tangu tukiwa wadogo na vile alivyojitahidi kupambana kutimiza ndoto zetu na zake, alieleza vile matamanio yake yalivyokuwa juu yetu wanae. Nikamsikiliza kwa makini, lakini nikamueleza kwamba nia yangu ni njema, nilimwambia nayaona mafanikio zaidi kwenye biashara kuliko katika ajira, lakini pia nikamkumbusha kwamba asisahau kwamba hali yake ya afya si nzuri kwa sasa ni wakati anaohitaji msaada wa karibu na msaada huo sio mwingine ni pesa kwanza. Isitoshe elimu ya chuo inasomwa wakati wowote ningeendelea wakati sahihi ambao sio huu. Hakuelewa. Hakuelewa kabisa.

Baada ya vuta nikuvute ya muda mrefu nikaona kwa kuendelea kushikilia msimamo wangu nitamuua huyu mama nikizingatia zaidi hali yake ya afya. Kama sitakuwa kuwa makini naweza kuamsha maradhi yake na huenda hali isitengemae tena na kupelekea mauti yake, itakuwa majuto kiasi gani? nikakubali kushindwa na nikamuahidi kwamba nitakwenda shule. Hapo uso wake ukachanua akafurahi sana.

Niliamua kumfariji tu, ahadi yangu haikuwa kweli. Dhamira ilikuwa palepale.

****

Siku ya siku iliwadia, nilikuwa natakiwa kuripoti chuo kikuu cha Dar Es Salaam almaarufu UDSM nikichukua mchepuo wa biashara. Nilichofanya ni kwamba pamoja na barua ya kujiunga na chuo ambayo ndio yenye orodha ya mahitaji muhimu, mimi nilimsomea tofauti na kile kilichoandikwa kwenye barua hiyo kwa

sababu mama yangu hajui kusoma na ananiamini sana, hivyo nikatumia udhaifu huo kutekeleza hadaa yangu. Nilimtajia gharama kubwa tu, si kwa kumkomoa, hapana. Ni kwa sababu nilijua hela ilipo.

Tangu tukiwa wadogo alikuwa akitupandia miti kila mmoja eneo lake, kule kwetu wazazi hupanda miti ambayo inakua taratibu kwa ajili ya watoto wao ili ije kuwasaidia kwa maisha yao ya baadaye. Sasa kila nikipanga mipango yangu 'haramu' siku zote macho yangu yalikuwa hapo, nilishaipigia hesabu kwa idadi na umri wake na kujua nikipasua mbao nikauza ni mtaji mzuri kabisa. Niliiona fursa. Nilijua wapi pa kuanzia.

Baada ya kumsomea mahitaji ya shule akashika tama na nilihakikisha anaona jinsi mzigo ulivyo mzito kiasi ambacho asipokuwa makini shule inanishinda, mawazo yakamjaa tele hajui wapi anapata pesa, hapo ndipo nikatumia mwanya huo kuingiza mawazo yangu kuhusu kuuza japo ekari moja ya miti yangu ili inisaidie kutimiza mahitaji ya shule. Hakupinga. Moyoni mwangu nikauona ushindi mnono.

"Tena fanya hima maana muda nao sio rafiki" Akasisitiza ili nitafute mteja haraka na biashara ifanyike.

Sikulaza damu haraka nikafanya michakato na mteja akapatikana nikaiuza ile miti, na bila kukawia nikamuaga kwamba sasa nakwenda shule, akanipa baraka zote nikaondoka zangu.

Kama nilivyopanga sikuenda chuoni kama nilivyoaga nyumbani. Nilipofika Iringa mjini safari ikabadilika badala ya kuelekea jijini Dar es salaam nikapanda gari kuelekea Njombe, wakati huo bado ilikuwa ni moja ya wilaya za mkoa wa Iringa. Yalikuwa maamuzi magumu mbayo mimi mwenyewe yalinitia hofu wakati kwa sababu nilijiona kabisa jinsi nilivyojitoa mhanga. Kitu pekee nilichotakiwa kuhakikisha sifanyi makosa nikurudi na hela nyumbani ili nieleweke na si vinginevyo. Najua nikifanikiwa ni rahisi kujieleza kuliko mambo yakienda ndivyo sivyo basi ningempoteza mama yangu katika dunia hii. Nilimuona ni mtu asiyehitaji mshtuko wowote kwa sasa kutokana na hali yake ya kiafya. Bila hivyo, ilikuwa kasheshe, mpaka sasa sijui ulikuwa uthubutu gani wa aina ile, nafikiri ni kwa sababu nililelewa kujiamini, hata hivyo niliongozwa na dhamira njema.

Baada ya kufika Njombe nikaunga urafiki na kijana aliyefahamika kwa jina la Amos kwa kuwa nilifahamu bila mwenyeji biashara ingeniwia vigumu sana. Sasa kwa kushirikiana na Amos nikafanikiwa kufanya tafiti ndogo kuhusu biashara ambayo ingenilipa kwa wakati, nikagundua shughuli maarufu hapa ni miti na viazi nikachagua ile ya miti ambayo kidogo nilikuwa na uzoefu nayo lakini sasa sikupanga kupanda tena maana ingekuwa biashara ya muda mrefu sana na mimi nahitaji faida ya haraka kukimbizana na muda nikaamua kununua miti na kupasua mbao kisha kuzisafirisha kwenda Dar, Iringa nikawa napapita kama mpita njia lakini kwa siri sana, sikutakiwa kufahamika na yeyote kwamba siko chuo ndio maana hata

nilipomuona mtu niliyemfahamu popote basi nilimkwepa vikali.

Biashara ziliendelea vizuri ingawa kuna wakati ziliyumba lakini nilipambana bila kukata tamaa nikiamini nina deni na nina kesi vilevile.

Kila hatua niliyonyanyua na kutua unyayo wangu nilikumbuka natakiwa kuiinua familia kiuchumi, pia natakiwa kurudi na hela nyumbani kwa kuwa tayari nimekacha shule kwa siri, kinyume na hapo itageuka dhahma ya hali ya juu. Lakini niliamini mambo yakikaa sawa nitamalizia shahada yangu. Nilichofanya ni kucheza na nyakati, nikawa narudi nyumbani mara chache, nilitegea likizo za vyuo ndio naonekana nyumbani ili kuleta uhalisia wa kiuanafunzi na vyuo vikifunguliwa tu narudi kwenye shughuli zangu wao wanajua nimerudi nikitokea shule. Maisha yakawa hayo.

Kwa msaada mkubwa wa Amos nilijikuta napata faida kubwa sana katika biashara yangu, nikampenda sana tukawa kama ndugu kutokana na uaminifu wake utafikiri tulifahamiana kabla ya hapa, alinishauri mambo mengi na hakika tulinyanyuka kwa pamoja. Kadri biashara zilivyokwenda tukashauriana sasa kuwekeza kwenye miti kwa sababu tuliona ni uwekezaji mkubwa wa baadaye. Kwa hiyo kiasi kikubwa cha pesa nikapeleka huko na kiasi kidogo kilichosalia nikapanda miche ya maparachichi ambayo sikuitilia maanani hata hivyo. Mimi niliweka pesa yangu nyingi kwa sababu nilichukua miti mikubwa ambayo baada ya muda mfupi napasua na kuuza mbao. Nililenga faida ya haraka.

Miaka ilienda haraka sana, biashara zangu zilienda vizuri, nilipanga nitengeneze pesa nyingi halafu nimshtukize mama, niliamini akiona mafanikio basi kesi ya kukacha masomo haitakuwa na mashiko tena. Napo ni ikiwa atagundua maana ilikuwa siri kubwa.

Siku, miezi, miaka ilikatika. Karibu miaka mitatu sasa ilikuwa imetimia, hesabu zangu ilikuwa lazima ziende sawasawa na miaka ya masomo, hatimaye miaka ya masomo ndio hiyo imeisha na mimi nikarudi mara moja nyumbani ili kuwapumbaza, Nilijitahidi kutumia akili wakati wote ili kufanya uhalisia wa mambo uende vile wanavyofahamu. Mama alifurahi sana akiamini nimehitimu masomo, nikakaa nyumbani kidogo kwa takribani wiki tatu nikadanganya kwamba wakati ambao nasubiri cheti inanilazimu kuondoka hapo nyumbani kwenda kutafuta pesa maana hakuna kilichobaki tena. Mama akakubali, hapo sasa alikuwa radhi bila mashaka. Nikaondoka kurudi Njombe.

Miezi ikasogea, kwa kawaida nikiwa huko huwa nakaa mashambani huko na mjini huwa nakwenda mara chache kwa shida maalum, baridi ilikuwa kali sana kama ada ya huu mji ukizingatia mazingira yenyewe mimi na wapambanaji wenzangu tuliishi katika vibanda tu kujisitiri.

Kuna tarehe nisiyoikumbuka almanusura nigeuke mwehu. Nikiwa nimejikunyata

kibandani kwangu usiku wa manane nikashtukia purukushani na mayowe ya watu huko nje, usingizi ukakata ghafla. Nikatega sikio kujua kinachoendelea, bado sikuelewa ikanilazimu kukurupuka mpaka nje. Lahaula!! Moto mkubwa ulikuwa umezuka ukiteketeza mashamba ya miti.

Sikusubiri, nikajitanda shuka almaarufu kama 'Masai' na kukimbilia moto ulikotokea. Huu mji wakati wa kiangazi kuna tatizo kubwa la moto kuunguza mashamba hasa kwa sababu hiyo miti inakamata moto kwa urahisi sana. Nilipofika nilijikuta miguu inakosa nguvu, macho yanapoteza uwezo wake. Nikakaa chini.

Sikumbuki nini kiliendelea pale lakini nilipafahamu zangu nikiwa kambini, inaonekana hakikupita kitambo kirefu tangu kuzirai mpaka kurejewa na fahamu zangu, nikavuta kumbukumbu vizuri, mara ya mwisho niliona moja ya mashamba yaliyokuwa yanawaka moto na langu ni mojawapo. Nikapoteza fahamu tena.

Nilikuja kurejewa na fahamu baada ya masaa kama mawili baadaye, tayari ilikuwa yapata saa mbili za asubuhi. Pembeni walikaa wapambanaji wenzangu akiwemo Amos, kule mashambani moto uliendelea kuwaka lakini ukimalizikia maana ulishamaliza kazi yake, watu walichofanikiwa ni kuzima usiendelee kuenea kwenye mashamba mengine, yale yaliyokamata moto miti iliteketea yote. Ekari yangu ilikuwa imeteketea kabisa nilibaki nimepigwa na bumbuwazi. Kulia siwezi, kucheka siwezi. Nilichoweza ni kusimama na kutazama eneo lililoteketea jinsi 'lilivyopendeza' kwa kazi nzuri ya 'bwana moto'

Mkosi ulioje!

Ziliibuka dhana mbalimbali juu ya chanzo cha moto ule, wapo waliosema wakati wa kiangazi moto unaunguza sana mashamba sababu ya nyasi kukauka ambazo hukamata moto kirahisi pindi unapowashwa kulingana na shughuli zinazoendelea mashambani ikizingatiwa kwamba miti hii ina asili ya mafuta mengi ndio sababu inadaka moto kirahisi. Wengine wakasema shamba lisiposafishwa kuzunguka eneo lake moto unaweza kuhamia kirahisi toka huko ulikowashwa kutokana na kukamata nyasi zilizomea kulizunguka kwa urahisi.

Na wapo waliodai wenyeji wanapouza hayo mashamba huwa wanauza kwa sababu wana shida baadaye wanapoona mafanikio huwa wanaingia kinyongo kwa hiyo huwa wanachoma makusudi. Yote hayo sikujisumbua kuyafikiria, pesa yangu imeteketea ndio nilichojua. Basi!

Kwa wiki nzima mfululizo nilibaki sijielewi, kama zumbukuku, haikuwa kawaida kiasi cha kuwashtua wapambanaji wenzangu sasa ikawa ni kibarua cha kunilinda popote ninapokwenda wakihofia huenda ningejinyonga. Walishtushwa kuona naweza kuwa mwehu ambacho hawakujua ni kwamba nimepoteza hela ambayo ndio tiketi yangu kurudi nyumbani. Amos alifahamu nimeweka pesa nyingi kiasi gani katika mradi huo ndio maana ilinigharimu muda mrefu kurudi katika hali yangu ya

kawaida. Baada ya muda akili ikatengemaa nikawa sawa kiasi chake.

Na sasa ndio nikapata wasaa kujiuliza naanzia wapi? Naishia wapi!? Nikirudi nyumbani nitaondokaje, nikiondoka naenda wapi? Muda wa kusubiri majibu ya chuo ukiisha nitaulizwa kuhusu cheti nitajibu nini? Angalau ningekuwa na pesa pasingekuwa na maswali mengi. Mchawi pesa, ningeweza kusema kweli nilikacha shule na isiwe kesi kwa kuwa hela ipo. Sasa kwa hali ilivyo sasa sina jeuri hiyo.

Kutokana na kuyumba kiuchumi ilikuwa ni lazima kurudi nyumbani, nisingeweza kuendelea kukaa porini. Sikuwa na pesa na sikuwa na kazi ya kufanya tena. Hayo mengine yatafahamika mbele ya safari, nikafunga safari mpaka nyumbani. Hakukuwa na maswali mengi kutoka kwa mama, alipojaribu kunidodosa nikamfahamisha tu kwamba mambo magumu huko nitokako na sikutaka maswali mengi.

Baada ya kukaa pale nyumbani kwa muda nikapata wazo jipya. Tabasamu likachanua usoni pangu, akili yangu ikaanza kufikiria zile ekari zingine za wadogo zangu. Nilikuwa nahitaji kufanya maamuzi magumu kwa mara nyingine tena lakini safari hii, hii ndio ilikuwa kete ya mwisho. Nikifeli tena ndio basi tena nimejimaliza na nimeimaliza familia nzima.

Kinyume na maamuzi ya mwanzo, haya ya sasa hata mimi yaliniogopesha zaidi. Kule Njombe sina kitu zaidi ya ekari chache za mashamba ya parachichi ambayo hayana tija sana. Kuhusu chuo nilidanganya hivyo sikuwa na cheti jambo ambalo nilifanikiwa kulifanya siri yangu, na hili la sasa kuuza miti ya wadogo zangu nikiangukia pua nitakuwa mgeni wa nani? Nikavuta pumzi ndefu na kuzishusha. Akili ilikuwa inavurugika. Nikapiga moyo konde.

"Mama hatimaye shule imekwisha" Nilianza kurusha ndoano.

“Unataka kusemaje?” Mama akarudisha swali kwangu. Safari hii hakuwa na mchecheto alinisikiliza kwa makini sana.

“Bado akili yangu inafikiria pesa” nikaendelea kumpanga, sasa nilikuwa huru bila woga.

"Kwa hiyo!??" Akauliza.

Nikafikiria kwa kitambo kidogo kisha nikaamua kumueleza namna gani tutauza ile miti ya wadogo zangu nikipata pesa nianze kufanya biashara yoyote kutoka mikoani kupeleka Dar. Nilitumia muda mrefu kidogo kumueleza jinsi biashara hivyo ilivyo na pesa ya kutakata. Safari hii tofauti na nilivyotegemea mama hakuwa na upinzani sana alikubali pendekezo langu kirahisi sana, lakini moyo ni mwangu niliumia, niliumia kwa kuwa niliona naweza kuwa sababu ya anguko lao wote. Sasa nitafanyaje na hakuna namna, nia yangu ilikuwa kurudi kwenye mstari kufuta machungu na historia mbaya. Hatimaye nikauza miti hiyo kwa mara nyingine.

Niliondoka kurudi Njombe nikiwa na mawazo tele namna gani nitaichekecha hii pesa ili nitimize malengo niliyojiwekea. Nilipanga kufanya biashara ya mazao lakini sio kupanda mashambani tena, nilishang'atwa na nyoka hata nikitembelewa na jani nashtuka, safari hii ilikuwa kununua na kuuza viazi ambapo niliambiwa soko zuri liko Dar na mikoa ya kusini yaani Lindi na Mtwara. Nikiwa ndani ya gari kurejea Njombe simu yangu ndogo iliita. Nikaitoa mfukoni na kutazama jina la mpigaji, alikuwa swahiba wangu, mpambanaji mwenzangu ambaye yeye alibakia huko tangu niondoke. Ni Amos!

Utafikiri alijua niko njiani kurejea uwanja wa mapambano. Pamoja na kwamba nilikuwa ndani ya gari nilipokea simu yake, tukaongea kwa kirefu sana, kwa kuwa nilikuwa ndani ya gari sikutaka mtu mwingine aelewe mazungumzo yetu, kwa hiyo nilikuwa nikiitikia tu na kuchombeza kwa maneno mara chache. Baada ya mazungumzo nilikata simu. Nikavuta pumzi ndefu na kuzishusha kama kawaida yangu. Ilikuwa taarifa nzuri na muhimu sana, ilinipa ahueni na morali upya.

Wakati nikiendelea na tafakuri ukaingia ujumbe mfupi katika simu yangu, nikafungua kikasha ilikuwa namba ya simu ambayo Amos aliahidi tukimaliza mazungumzo atanitumia namba ya mtu ambaye nikifika natakiwa nimtafute. Nilijilaumu Kwa nini niliuza miti ya wadogo zangu kama ningejua ningeachana nayo maana hela ilikuwa njiani.

Nilipofika Njombe baada ya kushuka garini tu sikutaka kupoteza muda nikaipiga ile namba, mpokeaji alikuwa raia wa Kenya kama ambavyo swahiba wangu alinifahamisha. Huyo mtu alikuwa ananunua zao la parachichi kwa wingi na kwa bei nzuri. Kwa maelezo ya swahiba wangu watu wameshatajirika ghafla na zao la parachichi limeadimika hivyo tuliobaki nayo tuko wachache sana na kwakuwa hapo awali parachichi lilikuwa zao lililopuuzwa hivyo wakulima wake tulikuwa wachache ndio sababu waliouza waliuza kwa pesa nzuri.

Simu iliendelea kuita ikiwa sikioni kwangu ningali wima na begi yangu ndogo mgongoni, ilipopokelewa nikajitambulisha kwa Mkenya, alifurahi sana na kwa bahati nzuri sehemu niliyokuwepo hapa kuwa mbali na alipokuwepo kwa wakati huo, akaja tukazungumza biashara na kwa kuwa alikuwa na usafiri wa gari binafsi tu kafunga safari mpaka mashambani siku hiyohiyo ili nikamuonyeshe. Bado sikuamini kama ni parachichi hilohilo lililodharauliwa na wengi ghafla nakwenda kupiga ‘bingo’ kimaajabu. Baada ya kumuonyesha tukakubaliana siku inayofuata ndio iwe siku ya malipo. Ukisikia kulala masikini na kuamka tajiri ndio hii sasa.

Kesho yake niliwahi mapema kabisa, nikakabidhiwa hundi ya takribani milioni arobaini ikijumlisha na mkataba mpya ambao waliniomba niwe wakala wa manunuzi lakini sharti lilikuwa lazima niwe na kampuni iliyosajiliwa ili mambo yasiende kienyeji. Kwanza ilinishtua, yaani mimi niwe na kampuni? Nawezaje? Maana niliona inahitaji kumiliki utajiri mkubwa sana ili kuwa na kampuni.

“Wasiwasi wako tu mtu yeyote anaweza kumiliki kampuni” Mkenya akaendelea kunitia moyo.

“Usina’mbie! ”

“Nitakuelekeza usijali” Mkenya akajibu halafu likafuata somo zito jinsi navyoweza kumiliki kampuni yangu mwenyewe pamoja na mtaji wangu mdogo. Ni hakika wenzetu wamefunguka sana akili katika masuala mengi sana.

Baada ya mazungumzo marefu tukaagana tukiweka miadi ya kuwasiliana mara tu nitakapokamilisha taratibu zote za usajili wa kampuni yangu.

Kwa mchecheto niliokuwa nao sikutaka kupoteza muda siku iliyofuata nilikuwa ndani ya basi nikilitafuta jiji la Dar Es Salaam ili kuanza mchakato wa kuanzisha kampuni hata rafiki yangu Amos sikumuaga tulikuja kuwasiliana baadaye sana.

Nikiwa safarini nikampigia simu mama yangu kumjulisha namna nilivyookota dodo chini ya mnazi, lakini simu haikupokelewa, nikaipiga tena akapokea mdogo wangu aliyenifuata nikapata mashaka;

“Mama yuko wapi?” nikaanza na swali moja kwa moja.

“Mama anaumwa sana tangu ulipoondoka” Akajibu.

Taarifa hii ikanitia katika simanzi maana nilimpenda mama yangu na nilimhurumia sana. Nikawalaumu Kwa nini hawakunijulisha, mdogo wangu akasema mama alishindwa kuniambia kwa sababu anajua sina pesa, pesa niliyokuwa nayo anajua ni mtaji wa biashara. Kwa jibu hili niliona kabisa jinsi upendo wa mama usivyo na mipaka. Mama alikuwa anaelekea kujitoa mhanga kwa ajili yangu, yuko tayari kufa mradi tu nisitumie pesa anayojua ni mtaji kwa ajili ya maisha yangu na wadogo zangu hapo baadaye.

Nikafikiri kwa kina kisha nikamtaka ampe simu niongee naye.

Japokuwa aliongea kwa tabu lakini naye akaniambia vilevile alivyosema mdogo wangu, nikamueleza namna hali yangu kiuchumi kwa sasa na kwamba niko safarini kuelekea Dar hivyo mambo yakikaa sawa nitashughulikia suala la matibabu yake. Naam sasa nilikuwa na jeuri ya kuongea chochote mbele ya yeyote, hata hali ya mama ikibadilika na kuwa mbaya sikuwa na mashaka kwa kuwa pesa ipo na uhakika wa matibabu upo vilevile. Wakazi wengi wa bara la Afrika kinachowaua ni umasikini wala si maradhi.

Hivyo ndio kampuni ilivyoanza, na ndivyo nilivyosimamia uhai wa mama yangu ambaye madaktari walisema alipata shida kwenye mfumo wa moyo. Kwa lugha nyepesi tungesema alikuwa na matatizo ya moyo sikumbuki kitaalamu walisema ugonjwa unaitwaje. Lakini haikuwa changamoto kubwa kwa kuwa pesa ilikuwepo kusimamia kila kitu.

****